



NCHI YETU

Jarida la Mtandaoni



TOLEO NA.2

Limeandaliwa na Idara ya Habari-MAELEZO


TOLEO LA FEBRUARI 2017

TUNATEKELEZA: Mabilioni Yamiminika Miradi ya Maendeleo

787 Dreamliner



Mchoro barabara ya juu Tazara



Mtambo wa Umeme wa Kinyerezi 1



Mtambo wa Maji Ruvu Juu





Bodi ya Uhariri

Mwenyekiti

Dkt. Hassan Abbasi

Mkurugenzi-Idara ya Habari-MAELEZO

Wajumbe

Zamarudi Kawawa

Vincent Tiganya

John Lukuwi

Elias Malima

Msanifu Jarida

Hassan Silayo

Benedict Liwenga

Huduma zitolewazo MAELEZO

1. Kuuzza picha za Viongozi wa Taifa na matukio muhimu ya Serikali.
2. Kusajili Magazeti pamoja na Majarida
3. Kukodisha ukumbi kwa ajili ya mikutano na Waandishi wa Habari.
4. Rejea ya Magazeti na Picha za Zamani
5. Kupokea kero mbalimbali za wananchi.

Jarida hili hutolewa na:

Idara ya Habari-MAELEZO

S.L.P 8031

Dar es Salaam-Tanzania

Simu : (+255) 22 -2122771

Barua pepe: maelezo@habari.go.tz

Tovuti: www.tanzania.go.tz



WATUMISHI HOUSING COMPANY

"Dhamana ya Uwekezaji katika Nyumba"



"Hamia kwako leo"

kwa mkopo wa nyumba wa bei nafuu.
Malipo ni ndani ya mwaka 1 hadi miaka 25.

Kwa sasa tunajenga na kuuza nyumba bora na kisasa maeneo mbalimbali nchini:

Kigamboni (Gezaulole) **Mwanza** (Kisesa)
Morogoro (Mkundi) **Bunju B** (Mabwepande Road)
Magomeni (Usalama Apartments)

PIGA SASA

0715 353 465 / 0757 437 594 / 0756 447 422



Kwa maelezo zaidi na kuweza kuchukua fomu za kununua nyumba tembelea ofisi zetu zilizopo jengo la Golden Jubilee Towers gholofa ya 4 au tembelea tovuti yetu.



@Watumishi Housing Company

www.whctz.org

TAHARIRI

HONGERA JPM KWA VITA DHIDI YA DAWA ZA KULEVYA

Hivi karibuni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli ameonyesha dhamira yake ya dhati ya kupambana na dawa za kulevya kwa kumteua Kamishna Rogers William Sianga kuwa Kamishna wa Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Dawa za Kulevya.

Akiongea mara baada ya kumwapisha Kamishna huyo, Rais Magufuli alimtaka Kamishna Sianga kupambana na dawa za kulevya bila ya kuogopa ili kuokoa nguvu kazi ya taifa inayoteketea kwa utumiaji wa madawa hayo

Katika kuonesha dhamira ya dhati ya kupambana na janga hili Rais Magufuli alisema ni vyema sasa vyombo vyote vya ulinzi na salama vikashirikiana kupambana katika vita hiyo ili kuondoa kabisa dawa hizo hapa nchini.

Kwa upande wake Kamishna Sianga alimuahidi Mh.Rais kufanya kazi kwa uaminifu ili kuweza kufanikisha azma ya Serikali ya kutokomeza biashara na utumiaji wa dawa za kulevya kwani zimekuwa zikipoteza nguvu kazi ya Taifa.

“Hatutajali mtu yeyote, hii vita ni kubwa hatuwezi kwenda nayo kwa mzaha hivyo nitasimamia sheria ili kuhakikisha dawa za kulevya zinabaki kuwa historia nchini,” alisema Kamishna Sianga.

Alisisitiza kuwa vita ndio kwanza imeanza kushika kasi, na itaendelea kupiganwa hadi imalizike hivyo Watanzania hawana budi kuunga mkono jitihada zinazofanywa na Serikali kwa kutoa ushirikiano kuhakikisha wanatokomeza uzalishaji, usambazaji, uuzaji na matumizi ya namna yoyote ya madawa ya kulevya, kila mmoja anatakiwa kushiriki kikamilifu katika vita hii ili hatimaye iweze kufanikiwa.

Sisi tunaamini kuwa vita hii ni ya haki na inapaswa kuwa ya kila mtanzania. Tumuunge mkono Rais pamoja na watendaji wapya aliowateua ili wafanikiwe. Ni jukumu pia la kila mwananchi mmoja mmoja pamoja na viongozi wa ngazi zote nao kushirikiana kwa pamoja katika kufanikisha vita hii.

TUNATEKELEZA: Mabilioni Yamiminika Miradi ya Maendeleo



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na Waziri wa Nishati na Madini, Profesa Sospeter Muhongo (kushoto kwake) wakitazama mfumo wa usambazaji umeme

Na Mwandishi Wetu

“TUNATEKELEZA” ndilo neno fupi lakini linalobeba uzito wa kazi kubwa inayoendelea kufanywa na Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Rais Dkt. John Pombe Magufuli. Mafanikio hayo makubwa yanakuja ikiwa ni takribani miezi 15 tu sasa tangu Serikali yake iingie madarakani.

Takwimu ambazo jarida hili limezipata zinaonesha kuwa mpaka kufikia Januari mwaka huu, ikiwa ni nusu ya mwaka huu wa fedha, miradi mingi ya maendeleo imeshapokea mabilioni ya fedha za utekelezaji. Hali hii inaonesha dhamira ya wazi ya Serikali.

Akiwasilisha baadhi ya takwimu hizo Bungeni mapema Februari, 2017, Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Phillip Mpango, amebainisha

kuwa Serikali katika kuhakikisha kuwa ahadi zilizoko katika Ilani ya Uchaguzi, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na zile za Rais, vinatekelezwa ipasavyo, inaendelea kuhakikisha kuwa fedha zilizotengwa zinatolewa ili kuinua maisha ya Watanzania.

Uchambuzi wa NCHI YETU unaonesha kuwa miradi mingi ya maendeleo kama vile maji (mijini na vijijini), usambazaji wa umeme, ujenzi wa barabara na miundombinu mingine, kilimo na miradi mingine mikubwa kama vile ununuzi wa ndege mpya za kisasa, yote imeendelea kupokea mabilioni ya fedha ili kuharakisha utekelezaji.

Ununuzi wa ndege mpya

Kwa mujibu wa takwimu hizo, Serikali imeshatumia kiasi cha shilingi bilioni 234.937 kwa ajili ya ununuzi wa ndege mpya

mbili aina ya Bombardier Q400 (ambazo zimeshawasili nchini na zimeanza kutoa huduma) na kiasi kingine ni malipo ya awali ya ununuzi wa ndege mpya nne (4).

Miongoni mwa ndege hizo nne mpya ambazo zitaanza kuwasili nchini mwishoni mwa mwaka huu na kukamilika mwakani ni ndege kubwa yenye uwezo wa kubeba abiria takribani 260 ya aina ya Boeing Dreamliner.

Umeme na Maji

Katika kuhakikisha wananchi hasa walioko vijijini wanaendelea kupatiwa huduma ya uhakika ya nishati ili kuinua maisha yao, takwimu hizo zinaonesha kuwa kiasi cha shilingi bilioni 267 kimeshatolewa ili kutekeleza miradi ya usambazaji wa umeme vijijini.

Katika sekta muhimu ya maji (mijini na vijijini) Serikali nako imeendelea kutekeleza ahadi zake kwa kutoa kiasi cha shilingi bilioni 165. Kiasi



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli akipata maelezo ya namna mandhari itakavyokuwa baada ya kuweka jiwe la msingi kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa barabara ya juu kwenye makutano ya barabara za Mandela na Nyerere eneo la Tazara Jijini Dar es Salaam

hicho kimesaidia kuendelea na kukamilika kwa miradi mingi ya maji mijini na vijijini itakayosaidia sana maisha ya wananchi.

Ujenzi wa Miundombinu

Si ndege, maji na umeme tu, ripoti ya hali ya uchumi ya nusu mwaka inaonesha kuwa Serikali ya Rais Magufuli pia imeshatoa kiasi kikubwa katika ujenzi wa barabara maeneo mbalimbali nchini. Tayari kiasi cha shilingi bilioni 916 kilishatolewa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu hii muhimu. Miundombinu mingine ambayo tayari imeshapewa fedha za kutekeleza miradi iliyopangwa ni: upanuzi viwanja vya ndege vya Dodoma na Mwanza (shilingi bilioni 12.352) na Mfuko wa reli (bilioni 58).

Elimu na Afya ni Nguzo Muhimu

Serikali kwa kutambua umuhimu wa sekta hizi, imeainisha Bungeni mapema Februari utoaji wa fedha za kutekeleza masuala mbalimbali.

Kuhusu afya, taarifa ya hali ya uchumi iliyowasilishwa na Dkt. Mpango inaonesha kuwa kiasi cha shilingi bilioni 235 zimetolewa kusaidia uboreshaji wa huduma za afya ikiwemo ununuzi wa dawa. Katika elimu tayari kufikia nusu ya mwaka wa bajeti, inaonesha ripoti hiyo, kiasi cha shilingi bilioni 277 kimeshatumika kwa ajili ya mikopo ya elimu ya juu na shilingi bilioni 124 zikiwa zimeshatumika kugharamia sera ya elimu bure.

Mbali ya sekta hizo, Serikali pia, inaonesha ripoti hiyo, imetoa mabilioni kugharamia masuala mengine muhimu ambapo, ukiacha mishahara na stahili muhimu za watumishi wa umma ambavyo vinaendelea kulipwa kwa wakati, masuala mengine muhimu pia yamepatiwa fedha kama ifuatavyo:

Ruzuku ya pembejeo (bilioni 10); ununuzi wa chakula cha hifadhi (bilioni 9); posho za mfuko wa jimbo na Mfuko wa Bunge (bilioni 35); michango ya taasisi

na Jumuiya za Kimataifa (bilioni 9.8); ruzuku kwa vyama vya siasa (bilioni 8.6) na uboreshaji wa shule zenye mahitaji maalum (bilioni 2.5).

Dhamira ya Rais Iko Wazi

Akieleza siri ya mafanikio haya makubwa katika kipindi kifupi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mhe. January Makamba, akichambua kwa ujumla utendaji na utekelezaji wa Serikali ikiwa ni miezi 15 tu madarakani, ameliambia bunge hivi karibuni, kuna mabadiliko makubwa katika kila eneo la utendaji wa Serikali ya Mhe. Rais Dkt. John Pombe Magufuli.

Waziri Makamba anayatathmini mafanikio yote haya kiutekelezaji akiyanasibisha na siri moja kubwa; dhamira safi na ya wazi ya Rais Magufuli kuenzi misingi aliyoiacha Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, misingi iliyoegama katika kuwatumikiawatu.



Ziara ya Rais Museveni Yafungua Milango ya Ushirikiano

Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli akimpokea mgeni wake Rais wa Uganda Yoweri Kaguta Museveni (kushoto) Ikulu Jijini Dar es Salaam, Rais Museveni alikuwepo nchini kwa ziara ya kikazi ya siku mbili.

Na Vincent Tiganya

Rais wa Uganda Mhe. Yoweri Kaguta Museveni amemhakikishia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli kuwa yupo tayari kuweka jiwe la msingi la mradi wa ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Hoima nchini Uganda hadi Bandari ya Tanga nchini Tanzania.

Rais Museveni alitoa kauli katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere Jijini Dar es Salaam wakati akiagana na mwenyeji wake Mhe. Rais Magufuli baada ya kumaliza ziara yake rasmi ya Kiserikali ya siku mbili

“Tulikuwa na mazungumzo mazuri na Mhe. Rais Magufuli,

tumejadili mambo mengi hususani kuhusu mradi wa ujenzi wa bomba la mafuta, tumekubaliana na Mhe. Rais mambo mengi, na sasa tutakwenda kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa mradi huo,” amesema Rais Museveni.

Awali Marais hao walikubaliana kutosaini mkatabawamahusiano ya kiuchumi na kibiashara kati ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na Ulaya (EPA). Hatua hiyo inatokana na kuonekana mkataba huo kutokuwa na faida bali ni aina nyingine ya ukoloni ambao unataka kurejeshwa kwa nchi za Afrika.

“Nimeongea na Rais Museveni amekubali kutosaini mkataba wa EPA, nitawaagiza wataalamu waliosaidia kutupa maelezo juu ya madhara ya mkataba

huo kwenda pia Uganda kuwapa maelezo ambayo waliyatoa kwa Tanzania,” alifafanua Dkt. Magufuli.

Kwa upande wake, Rais Museveni alisema kuwa ameongea na Rais Magufuli na wamekubaliana kutosaini mkataba huo na kuongeza kuwa suala la EPA ni lazima lijadiliwe na nchi zote za Afrika Mashariki ili kuwepo na msimamo wa pamoja kwa nchi zote za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Aidha Rais Museveni alimpongeza Rais Magufuli kwa kulifufua Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) kwa kununua ndege mpya Sita, hivyo amekaribisha shirika hilo kutoa huduma za usafiri wa anga nchini Uganda kutokana na nchi hiyo kuwa na uhitaji wa huduma hiyo.



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Balozzi Dkt. Augustine Mahiga (kulia) na Waziri wa Mambo ya Nje wa Uganda Oryem Henry Okello

Vilevile alimpongeza Rais Magufuli kwa ujenzi wa Reli ya Kiwango cha Kimataifa (Standard Gauge Railway) kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza na Isaka mpaka Rwanda ambapo itasaidia ujenzi wa bandari kavu katika Mkoa wa Mwanza hivyo wafanyabiashara wa Uganda kunufaika na bandari hiyo ambayo itakuwa karibu zaidi kuliko ilivyo kwa Dar es Salaam.

Wakati huo huo Rais Museveni alitoa wito kwa wafanyabiashara wa Kitanzania kwenda kuwekeza nchini Uganda mara baada ya kutembelea viwanda vya Kampuni ya Bakhresa vinavyozalisha Unga na Juisi vya Buguruni na Vingunguti jijini Dar es Salaam. “Nawakaribisha wafanyabiashara wa Kitanzania kuja nchini Uganda kuwekeza kwani kufanya hivyo kutasaidia kuzalisha bidhaa, upatikanaji wa soko pamoja na ajira”

alisema Rais Museveni.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa Mahusiano wa Kampuni za Bakhresa Hussin Sufiani alisema kuwa Kampuni hiyo hivi sasa ina kiwanda kimoja nchini Uganda ambacho kinazalisha unga wa ngano tani 1,100 kwa siku.

Alisema kuwa lengo ni kutaka kuongeza uzalishaji kutoka tani 1,100 hadi kufikia 2,000 ambapo uwekezaji huo umetoa ajira 650 kwa Waganda.

Kwa upande wa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji Mhe. Charles Mwijage anasema Uganda na Tanzania zimeingia makubaliano ya ushirikiano katika sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya viwanda.

Amesisitiza Watanzania wanaweza kwenda kuwekeza nchini Uganda kwa vile nchi hiyo inalima tani milioni 4 za mahindi lakini ina uwezo

wa kutumia tani milioni moja pekee, hivyo ni fursa kwa wafanyabiashara wa Kitanzania kwenda kuwekeza nchini humo.

“Tunawahamasisha wafanyabiashara wa Uganda na Tanzania kuwekeza katika nchi zao ili kuzalisha, bidhaa na ajira za kutosha kwa wananchi” alisema Waziri Mwijage.

Waziri Mwijage alitoa Wito kwa Watanzania kushiriki katika uchumi wa viwanda kwa kufanya uzalishaji wa bidhaa zinazotumika viwanda mfano kwa kulima matunda au mbogamboga.

Rais Yoweri Museveni aliwasili nchini jana kwa ziara ya kiserikali ya siku mbili ambapo akiwa nchini alifanya mazungumzo na Mwenyeji wake Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli na kutembelea Viwanda vya Said Salim Bakhresa vya Tazara na Vingunguti.

“Nimeongea na Rais Museveni amekubali kutosaini mkataba wa EPA, nitawaagiza wataalamu waliosaidia kutupa maelezo juu ya madhara ya mkataba huo kwenda pia Uganda kuwapa maelezo ambayo waliyatoa kwa Tanzania,” alifafanua Dkt. Magufuli.

Bonde la Mto Nile Muhimu kwa Uchumi wa Tanzania



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan akizungumza wakati wa sherehe za Siku ya Mto Nile hivi karibuni Jijini Dar es Salaam.

Na Jacqueline Mrisho

Maadhimisho ya 11 ya Siku ya Nile kwa mwaka huu yamefanyika nchini Tanzania kwa ushirikiano wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji pamoja na Sekretarieti ya Nile Basin Initiative (NBI) ambapo mgeni rasmi wa maadhimisho hayo alikuwa Makamu wa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan.

Maadhimisho hayo yalihudhuriwa na watu zaidi ya 600 wakiwemo Mawaziri wa nchi wanachama kutokakwenyenchihusika, mabalozi mbalimbali, wabunge, watu kutoka taasisi na mashirika mbalimbali pamoja na wanafunzi wa shule za Msingi, Sekondari na Vyuho Vikuu. Mto Nile ni miongoni mwa mito mikubwa iliyopo upande wa

Mashariki ya Bara la Afrika na Duniani kote ukiwa na urefu wa kilomita 6,695 ambapo beseni ya Nile hukusanya maji ya eneo linalojumuisha 10% za eneo la Afrika yote.

Mto huo ambao unaanzia Ziwa Victoria nchini Tanzania, ni chanzo kikubwa cha maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, viwandani, kilimo cha umwagiliaji na kuzalisha umeme kwa wakazi wa nchi za bonde hilo.

Kutokana na nchi nyingi kuzungukwa na mto Nile, suala la ushirikiano katika kusimamia na kuendeleza rasilimali za Bonde la Mto huo limepewa kipaumbele ili kuzuia migogoro inayoweza kuzuka baina ya nchi ambazo wanatumia mto huo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi inayosimamia shughuli za wanachama wa Bonde la Mto Nile (NBI), Innocent Ntabana anasema kuwa azma ya kusimamia na kuendeleza rasilimali za Bonde la Mto Nile limepewa kipaumbele na nchi zote zinazozungukwa na mto huo, jambo hilo ndilo limesababisha kuanzishwa kwa Sekretarieti ya NBI mwaka 1999 jijini Dar es Salaam.

“NBI ina jukumu la kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji za Bonde la Mto Nile kwa niaba ya nchi wanachama zipatazo 10 ambazo ni Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Ethiopia, Sudan, Sudan ya Kusini, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Misri,” anasema Ntabana.

Kwa upande wa Mratibu wa Kanda



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan akipata maelezo kuhusu Miradi mbalimbali inayotekelezwa kupitia Program ya Nile Basin Initiative alipotembelea mabanda ya taasisi mbalimbali wakati wa sherehe za Siku ya Mto Nile hivi karibuni Jijini Dar es Salaam.

wa Kitengo cha Uratibu cha Bonde la Mto Nile (NELSAP-CU), Elicad Nyabeeya anasema mto huo una manufaa makubwa kwa nchi wanachama kwani muunganiko wa nchi hizo umeleta mawasiliano mazuri ambayo yanapelekea kuinua uchumi wa nchi hizo pia kwa upande mwingine uwepo wa ushirikiano huo umesaidia nchi wanachama kufahamu tamaduni za watu tofauti tofauti.

Nyabeeya anasema “Tanzania inafaidika kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na NBI kupitia utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwemo miradi ya ujenzi wa bwawa la Bisrawi na usanifu wa bwawa la Borenga, mkoani Mara”.

Kwa mujibu wa Nyabeeya, Tanzania itanufaika na miradi ya maji na nishati ya umeme, pamoja na miradi mingine mingi ambayo NBI inaendelea kuitekeleza kama vile ujenzi wa mradi wa kuzalisha

umeme wa Rusumo na umwagiliaji katika mabonde ya mito Kagera na Ngoni iliyopo mkoani Kagera.

Anaendelea kufafanua kuwa mradi wa umeme wa Rusumo utazalisha megawati 80 za umeme ambazo zitatumwa na nchi za Tanzania, Rwanda na Burundi ambapo Tanzania inatarajiwa kupata megawati 16. Miradi mingine ni ya kuunganisha umeme kutoka Ethiopia, Kenya hadi Tanzania ikiwa ni pamoja na mradi wa umeme kati ya Tanzania na Zambia.

Aidha, NBI wanatarajia kukamilisha upembuzi yakinifu wa kina wa miradi ya Mara na Ngoni ifikapo mwezi Aprili mwaka huu ambapo wananchi 20,000 pamoja na hekari 13,630 katika vijiji 21 vinatarajiwa kunufaika na mradi wa Ngoni wakati Bonde la Mara litanufaisha wanachi 10,000. Miradi hiyo itahusisha usambazaji wa maji kwa

ajili ya matumizi ya majumbani, mifugo na shughuli za umwagiliaji.

Wakati huo, Bwawa la Borenga litakuwa likisambaza maji katika Bonde la Mara kwa wakazi wa vijiji 13 kwa ajili ya umwagiliaji na 17 vitapata maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na mifugo. Madhumuni ya miradi hiyo ni kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa maji ya uhakika, kuimarishwa kwa soko na mahusiano na kukuza sekta binafsi, kilimo, usalama wa chakula na kupunzuza umaskini.

Tanzania inafaidika kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na NBI kupitia utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwemo miradi ya ujenzi wa bwawa la Bisrawi na usanifu wa bwawa la Borenga, mkoani Mara”



Waziri Mkuu Mhe.Kassim Majaliwa akizungumza na Mawaziri na Wajumbe wa Baraza la Taifa la Udhibiti wa Dawa za Kulevya Nchini wakati akifungua kikao cha Baraza hilo leo Jijini Dar es Salaam.

Na Daudi Manongi

Undwaji wa Mamlaka ya Kupambana na Dawa za Kulevya ulifuatiwa na kuundwa kwa Baraza la Taifa la Kudhibiti Dawa za Kulevya ambalo lina wajibu mkubwa wa kutekeleza vita dhidi ya biashara hii haramu kwa vitendo.

Baraza hilo limeanzishwa chini ya kifungu cha 5 cha Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya namba 5 ya mwaka 2015 Kwa mujibu wa Sheria Waziri Mkuu ndiye Mwenyekiti wa Baraza hilo akiwa na wajumbe wengine 11.

Wajibu wa Baraza hili ni kusimamia utekelezaji wa Sera ya udhibiti wa dawa za kulevya nchini. Aidha Serikali imefanya jitihada mbalimbali katika kupambana na Biashara hii haramu ya madawa ya kulevya ambapo awamu zote zimefanya jitihada kubwa ambapo mwaka 1995 Sheria ya Kupambana na Dawa za Kulevya

ilitungwa na kuanzishwa Tume ya kuratibu na kudhiti dawa za kulevya ambapo sheria hiyo ilitumika hadi mwaka 2015.

Pia kilianzishwa kikosi kazi chenye wadau kutoka vyombo vya usalama na tume yenyewe ambapo kikosi kazi kilifanya kazi nzuri ya kukamata dawa za kulevya na kudhibiti kwa kiasi kikubwa waingizaji wa dawa za kulevya.

Kipindi cha Januari 2015 hadi Desemba 2016 vyombo vya dola vilikamata kiasi cha kilo 77 za heroin zikihusisha kesi 703 na kilo 32.3 za cocaine zikihusisha kesi 259. Mbali na hayo kilo 78,656 za bangi zilikatwa zikihusisha kesi 14323 na ekari 71 za mashamba ya bangi ziliteketezwa pmaoja na mirungi kilo 31463.615 ilikatwa ikihusisha jumla ya kesi 2362. Serikali imefanya mafunzo kwa watendaji wa vyombo vya udhibiti vilivyopo mipakani kuhusiana na njia za usafirishaji wa dawa za kulevya, sheria mpya

namba 5 ya mwaka 2015 ya udhibiti wa dawa za kulevya na matumizi ya vifaa vya utambuzi wa awali wa dawa za kulevya.

“Serikali imeendelea kutoa matibabu kwa kutumia dawa ya methadone kwa watumiaji wa dawa za kulevya aina ya Heroin na pia watumiaji zaidi ya 2223 wanapata huduma za matibabu katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Mwananyamala na Temeke” alisema Mhe.Kassim Majaliwa alipokua akizindua Baraza la Taifa la kudhibiti dawa za kulevya.

Pia alisema huduma za nyumba za upataji nafuu zipatazo 11 kwa Tanzania Bara zinatolewa na hadi sasa zimehudumia waathirika wapatao 2325 na kwa upande wa Zanzibar kuna nyumba 12 ambazo hadi sasa zimehudumia wathirika wapatao 7953. Aidha watuhumiwa mbalimbali wa Dawa za Kulevya wamepelekwa mahakamani ambapo Mahakama Kuu ya Tanzania imetoa hukumu

kwa kesi kubwa za dawa za kulevya zilizowahusisha wafanyabiashara wakubwa zikiwemo kesi ya jinai namba 47/2011 iliyowahusu watuhumiwa Fred William Chonde na wenzake ambao walihukumiwa kifungo cha miaka 20 jela na faini ya shilingi bilioni 15.

Pili kesi ya jinai namba 87/2011 iliyomhusu mtuhumiwa Said Kimaro ambaye alihukumiwa kifungo cha miaka 20 jela na faini ya mara tatu ya thamani ya dawa zilizokamatwa. Kesi ya jinai namba 53/2011 iliyowahusu watuhumiwa chukwudi

denis na wenzake ambao walihukumiwa kifungo cha miaka 30 jela kila mmoja na kulipa faini ya shilingi bilioni 3 kila mmoja na kesi ya jinai namba 91/2011 iliyomhusu mtuhumiwa miteka Godfrey Mwandamele amaye alihukumiwa kifungo cha miaka 20 jela na faini ya mara tatu ya kiasi cha dawa zilizokamatwa. Serikali inaendelea na vita hii dhidi ya wauzaji na watumiaji wa madawa ya kulevya na ni wito kwa wananchi kushirikiana na Serikali katika kulitokomeza

kabisa suala hili kwa pamoja.

Jitihada hizi za serikali ya awamu ya tano hazina budi kuungwa mkono na wadau wote wa kupamabana na biashara hii haramu kwa manufaa ya kunusuru kizazi cha watanzania waoateketea katika janga hili.

UNESCO Yamuunga Mkono JPM Vita Dawa za Kulevya

Na Judith Mhina

Shirika la Kimataifa la Elimu Sayansi na Utamaduni UNESCO Tanzania limeadhimia kuwajengea uwezo wa Waandishi wa Habari nchini ili kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kwa kufuata Sheria Kanuni na taratibu zinzosimamia taaluma yao.

Hayo yamesemwa na Kaimu Katibu Mtendaji wa UNESCO Taifa Dkt. Moshi Kimizi katika uzinduzi wa Kamati ya Kimataifa ya Mpango wa Maendeleo ya Mawasiliano – IPDC iliyokutana Magogoni Jijini Dar-es-hivi karibuni.

Akizindua Kamati hiyo Dkt Kimizi alisema, Kamati ya Kimataifa ya Mpango wa Maendeleo ya Mawasiliano, ina jukumu kubwa la kuelimisha, kuleta mageuzi na maendeleo katika mawasiliano. Shirika hilo limedhamiria kuwajengea wanahabari uwezo katika nyanja za uhuru wa upatikanaji wa habari bila vikwazo,

pia kuwawezesha Waandishi wa Habari, kumudu majukumu yao na kuhakikisha haki ya mwanahabari ya kufanya kazi yake kwa weledi bila kubughudhiwa inaenziwa.

Kamati ya kitaifa ya mpango wa mawasiliano inaundwa na wajumbe saba ikiongozwa na Mwenyekiti Dkt. Eva Solomon Msangi, Mhadhiri kutoka Shule Kuu ya Mawasiliano ya Chuo Kikuu cha Dar-Es-Salaam, na wengine wanne ambao ni, mjumbe mmoja kutoka Wizara za Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wadau muhimu wa Habari kutoka Baraza la Habari Tanzania – MCT na Media Institute of Southern Africa – Tanzania - MISA TAN pamoja na Wawakilishi wawili ikitoka UNESCO.

Dkt Kimizi aliwajulisha wajumbe kuwa wanajukumu la kuhakikisha sauti za waliopembezeni au waliosahaulika zinasikika, hivyo, Kamati inapopanga mipango yake iweke kipaumbele kwa kutenga rasilimali kwa ajili ya kuwajengea

uwezo, pamoja na kuwaimarisha ili waweze kutoa habari na kupata habari bila vikwazo. Akitoa taarifa ya Kikao cha Paris Ufaransa kwa kamati hiyo ya mpango wa mawasiliano Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Dkt Eva Msangi alisema kikao kilisisitiza juu ya Usalama, ulinzi dhidi ya Waandishi wa Habari uimarishwe na kuzingatiwa, kwa kuwa Waandishi wengi duniani wako katika hatari ya kuteswa au kuuwawa wakati wakitekeleza wajibu wao.

Dkt Msangi aliongeza kuwa baraza la Maendeleo la Mawasiliano la Dunia lilipendekeza na kuchagua mwenyekiti ambapo BiAlbana Shala kutoka Netherlands alichaguliwa kuendelea kwa kipindi kingine cha miaka minne. Katika kuweka uwiano wakijiografia wa Baraza, washirika wote wa UNESCO huwekwa katika makundi ya kikanda au kijiografia.



Bilioni 177.4 Kubadili Ubungo Kwa Barabara za Juu.



Muonekano wa Barabara ya juu (fly over) ya Ubungo (Ubungo Road interchange)

Na Mwandishi Wetu

Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi wa Rais John Pombe Magufuli kupitia Wakala wa Barabara nchini (TANROADS), hivi karibuni ilisaini mkataba na kampuni ya M/S China Civil Engineering Construction Cooperation kutoka China (CCECC) kwa ajili ya ujenzi wa barabara za Juu 'Interchange' katika makutano ya barabara ya Sam Najoma na Mandela Ubungo jijini Dar es salaam.

Hatua hiyo inalenga kuondoa msongamano wa magari katika makutano ya Ubungo.

Chini ya Mkataba huo, Mkandarasi kutoka Kampuni ya CCECC ya China kuanza ujenzi huo mara moja na ujenzi huo unatarajiwa kutumia takriban miezi 30

hadi kukamilika kwake.

Akizungumza mara baada ya kusaini mkataba huo Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara nchini TANROADS Mhandishi Patrick Mfugale alisema kuwa zaidi ya shilingi Bilioni 177.4 zinatarajiwa kutumika katika ujenzi huo utakaowekewa jiwe la msingi mwezi machi mwaka huu.

“Hakikisheni mnaanza ujenzi mara moja kwani Serikali imeshakamilisha taratibu zote na tayari kiasi cha shilingi bilioni 2.1 kimelipwa kwa ajili ya fidia kwa wananchi walioguswa na mradi huo” alisema Mhandishi Mfugale.

Ujenzi wa Ubungo interchange unajengwa kwa fedha ya mkopo kutoka Benki ya Dunia ambapo Serikali kwa upande wake imeshalipa fidia ya zaidi ya shilingi bilioni 2.1.

“Zaidi ya magari 65,000 yanapita kila siku katika makutano ya barabara za morogoro, Mandela na sam nujoma eneo la Ubungo hali inayosababisha msongamano katika barabara ya Morogoro ambayo ndio lango kuu la kuingia jijini Dar es salaam hivyo ufanisi wa mradi huo utahuisha hali ya usafirishaji katika jiji la Dar es salaam na kuchochea ukuaji wa uchumi” alisisitiza Mhandishi Mfugale.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya CCECC Bw, Jiang Yigao amemhakikishia Mhandisi Mfugale kuwa wataanza maandalizi ya ujenzi huo mara moja na watafanya kazi hiyo kwa wakati.



Dkt. Abbas: Maafisa Habari Tangazeni Mafanikio ya Serikali

Mkurugenzi wa Habari na Msemaji Mkuu wa Serikali, Dkt. Hassan Abbas akizungumza na Maafisa Habari na Tehama wakati wa Mafunzo elekezi ya matumizi ya tovuti katika Mikoa na Halmashauri za Wilaya nchini yaliyofadhiliwa na Shirika la Misaada la Marekaani (USAID) na kusimamiwa na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Wakala ya Serikali Mtandao. Mafunzo hayo yalianza tarehe 9-20 Februari, 2017, kulia ni Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Ofisi ya Rais -TAMISEMI, Rebecca Kwandu.

Na Ismail Ngayonga

Maafisa Habari na Mawasiliano katika sekretarieti za Mikoa na Halmashauri za Wilaya nchini wametakiwa kujitokeza na kuwajibika kikamilifu ili kuwawezesha waajiri wao kutambua wajibu na majukumu yao ya msingi katika kutangaza shughuli na mafanikio ya Serikali katika maeneo yao ya kazi.

Rai hiyo imetolewa hivi karibuni Jijini Mwanza na Mkurugenzi wa Habari na Msemaji Mkuu wa Serikali, Dkt. Hassan Abbas alipokuwa akizungumza na Maafisa Habari na TEHAMA katika mafunzo elekezi ya tovuti yanayofadhiliwa na Shirika la Misaada la Marekani (USAID) na kusimamiwa na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo pamoja na Wakala ya Serikali Mtandao (EGA).

Kwa Mujibu wa Dkt. Abbas alisema katika ulimwengu wa sasa suala la teknolojia ni jambo lisiloupekika,

hivyoniwajibuwa Afisa Habari kutmia nyenzo za kisasa za mawasiliano ikiwemo tovuti ili kuhakikisha kuwa wananchi na wadau wa maendeleo wanapata taarifa sahihi na zilizingatia wakati.

“Zipo taarifa za miradi mbalimbali ambayo Serikali imeifanya, pamoja na taarifa za bajeti za halmashauri ambazo wananchi watanapenda kuzifahamu, hivyo ni wajibu wenu Maafisa Habari kuweka taarifa hizi” alisema Dkt. Abbas.

Aidha aliongeza kuwa ni wajibu wa kila Afisa Habari aliyopo katika Mkoa na Halmashauri nchini aweze kujiwekea malengo ya utekelezaji ili aweze kujitafakari kwa kuwa kupitia malengo hayo ataweza kutatua changamoto mbalimbali zinazomkabili katika eneo lake la kazi.

Akifafanua zaidi Dkt. Abbas alisema ili kufikia malengo hayo

Maafisa Habari hawana budi kutengeneza mtandao wa mawasiliano baina yao ili kuwawezesha kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili katika maeneo yao ya kazi.

Dkt. Abbas alisema Serikali inatambua changamoto mbalimbali zinazowakabili maafisa Habari katika maeneo yo ya kazi, ambapo baadhi ya changamoto hizo zimeanza kupatiwa ufumbuzi ikiwemo suala la miongozo ya majukumu ya Afisa Habari na Mawasiliano.

Kwa Upande wake, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini katika Ofisi ya Rais- TAMISEMI, Rebecca Kwandu alisema katika mafunzo hayo yaliyotolewa kwa Maafisa Habari na TEHAMA yatasaidia kwa kiasi kikubwa kujibu hoja na kero mbalimbali za wananchi ambazo zimekuwa zikiwasilishwa mara kwa mara katika halmashauri mbalimbali nchini.

TANZANIA FEBRUARI HII



Mkuu wa Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) Generali Venance Mabeyo akila kiapo cha utii mbele ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli Ikulu jijini Dar es Salaam. Katikati ni Katibu Mkuu Kiongozi Balozi John Kijazi.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Spika wa Bunge Job Ndugai na Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Profesa Makame Mbarawa wakibonyeza kitufe kuzinduzi teknolojia ya 4G LTE ya Kampuni ya (TTCL) hivi karibuni Mkoani Dodoma. Kulia ni Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa TTCL Bw. Waziri Kindamba



Makamu wa Rais Mama Samia Suluhu Hassan akionyesha tuzo aliyokabidhiwa wakati wa sherehe za Siku ya Mto Nile Jijini Dar es Salaam. Sherehe hizo zimeshirikisha takribani nchi 10 zinazozunguka mto Nile




Baadhi ya wafanyakazi wa Wizara ya Afya wakishusha vifaa vya ofisi mjini Dodoma vikitokea Jijini Dar es Salaam, kutekeleza ahadi ya Serikali ya kuhamia Makao Makuu ya nchi, Dodoma

NCHI YETU KATIKA HISTORIA



Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere akishiriki shughuli ya ujenzi katika kijiji cha Ujamaa wakati wa uongozi wake



Aliyekuwa Waziri Mkuu Hayati Rashid Mfaume Kawawa akiweka mchanga kwenye mashine ya kufyatulia matofali wakati akiwa madarakani.



Rais Ali Hassan Mwinyi akimsindikiza Baba Mtakatifu, Papa John Paul II baada ya kuhutubia katika viwanja vya Jangwani



Hayati Makamu wa Rais, Dkt. Omar Ali Juma(kulia) akiwa na aliyekuwa Rais wa Afrika Kusini, Mzee Nelson Mandela pamoja na mkewe Winnie Mandela walipokuja nchini Februari 1990

Treni ya Umeme Kuchagiza Mageuzi Awamu ya Tano



Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni Hodhi Miliki ya Rasilimali za Reli (RAHCO), Masanja Kadogosa (wa tatu kutoka kulia), akibadilishana Mkataba wa awamu ya kwanza ya ujenzi wa reli ya Kisasa (Standard Gauge), na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Mota-Engil Africa, Bw. Manuel Antonio Mota

Na Benjamin Sawe

Tanzania imedhamira kufikia uchumi wa kati na ifikapo mwaka 2025 ikiwa itawekwa miundombinu bora.

Wizara ya ujenzi ambayo imepewa jukumu la kusimamia sekta ya ujenzi, uchukuzi na mawasiliano ambazo ni kichocheo muhimu cha maendeleo ya kiuchumi na kijamii hapa nchini imejikita katika kuboresha miundombinu hasa reli na barabara.

Akishuhudia utiaji saini uliofanyika jijini Dar es Salaam, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Prof. Makame Mbarawa anasema ujenzi wa reli ya kati itakayotumia treni za umeme na kwenda kwa spidi ya kilometa 160 kwa saa ni mafanikio makubwa.

Anasema ujenzi wa reli hiyo utaongeza chachu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii na kubainisha kuwa safari Dar es Salaam hadi Morogoro itatumia muda wa saa 1.16, wakati Dar es Salaam hadi Dodoma itatumia muda wa saa 2.30 na safari ya Dar es Salaam hadi Mwanza itatumia muda wa saa 7.30.

”Tunataka kuifanya nchi yetu iwe ndogo kwa kutumia miundombinu ya kisasa ndio maana serikali imeamua kujenga reli hii itakayotumia umeme na kwenda spidi kubwa kuliko nyingine zote Barani Afrika,”amesema Prof. Mbarawa. Naye Balozi wa Uturuki nchini

Yassemen Eralp, aliaidi kuendeleza ushirikiano na Serikali katika mradi huo mkubwa na kupongeza uongozi wa Serikali ya Awamu ya Tano katika kufanikisha

maendeleo kwa wananchi wake. Nchi za Ethiopia na Djibouti tayari zimezindua reli ya kisasa ya treni za kutumia nguvu za umeme ambayo inaunganisha Mji Mkuu wa Addis Ababa na mji wa Bandarini wa Djibouti.

Ni wazi kwamba Serikali ya Awamu ya Tano imedhamiria kuboresha huduma za biashara kupitia sekta ya usafirishaji, hivyo kila mwananchi anapaswa kuunga mkono juhudi zinazofanywa na Serikali katika kutatua changamoto mbalimbali.

Nchi nyingine zenye treni zinazotumia umeme mbali na Ethiopia na Djibouti ni pamoja na Misri ambayo ina mtandao mkubwa wa reli za aina hiyo. Ni usafiri ambao ni wa uhakika na wa haraka hivyo kuwa kichocheo kikubwa katika ukuajia wa uchumi.

Bilioni 18 Kutumika Kumaliza Changamoto ya Maji Dar



Moja ya Mtambo unaotumika katika uchimbaji Visima Virefu katika eneo la Kimbiji, mradi utakaosaidia kutatua changamoto ya upatikanaji wa maji katika jiji la Dar es salaam.

Na Frank Mvungi

Serikali kupitia Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam (DAWASA) inatekeleza mradi wenye thamani ya bilioni 18 unaolenga kuondoa changamoto ya upatikanaji wa maji katika Jiji la Dar es salaam.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Mkurugenzi wa Ufundi na Uendeshaji wa Mamlaka hiyo, Bw. Romanus Mwangi'ngowakati wa ziara ya waandishi wa habari katika eneo la Kimbiji ambako mradi huo unatekelezwa.

“Mkandarasi anaendelea na kazi na amelea mabomba yote na amechimba visima 15 ambavyo vitazalisha maji yatakayotumika katika Jiji la Dar es Salaam na mradi unatarajiwa kukamilika Machi

2017”, alisema Mwangi'ngo. Aliongeza kuwa utekelezaji wa mradi huo umefikia asilimia 85 na utakapokamilika maeneo ya Kigamboni, Temeke, Ilala na Jiji la Dar es Salaam kwa ujumla yatanufaika kwa kupata huduma ya maji safi na salama.

Kwa upande wa miradi mingine kama ule wa ujenzi wa Bomba kutoka Ruvu juu hadi Kimara ulikamilika mwezi Oktoba 2016 na uzalishaji wa majaribio unaendelea kwa ufanisi mkubwa, alisema.

Mradi huo wenye thamani ya dola za marekani milioni 59 ni moja ya mikakati ya Serikali katika kuhakikisha kuwa wakazi wa Jiji la Dar es Salaam wanapata huduma ya maji safi na salama na kuondokana na changamoto hiyo.

Aidha mradi huo utawezesha kiwango cha maji kufikia lita milioni 196 kwa siku kutoka lita milioni 82 za awali. Kwa upande wake, Bw. Salum Hamis mkazi wa Mbagala amepongeza miradi ya maji inayotekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na wananchi kwa kuwa imekuwa chachu ya maendeleo katika maeneo yao.

Aliongeza kuwa miradi hiyo imepunguza tatizo la maji na imewawezesha wananchi kutumia muda mwingi katika shughuli za kiuchumi na hivyo kuchochea ukuaji wa uchumi.

Katika kukabiliana na tatizo la miundombinu ya maji taka katika Jijila Dares Salaam mamlaka hiyo iko katika mchakato wa kuanza ujenzi wa mtambo mkubwa wa kuchuja maji taka katika eneo la Jangwani na kuboresha mfumo huo katikati ya Jiji.

Mradi mwingine ni ule wa upanuzi wa Ruvu Chini ambao umekamilika kwa asilimia mia moja na utawezesha upatikanaji wa maji kufikia lita milioni 270 kwa siku kutoka milioni 180 kabla ya mradi huo haujatekelezwa.

Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam (DAWASA) inajukumu la kumiliki miundombinu ya maji safi na maji taka kwa niaba ya Serikali, kusimamia utoaji wa huduma ya maji safi na maji taka Dar es Salaam, kugharimia, na kupanga mipango ya kusimamia upanuzi wa huduma pamoja na kuishauri Serikali kuhusu masuala ya huduma ya maji safi na maji taka Jijini Dar es Salaam

Serikali Yabadili Maisha ya Wenye Mahitaji Maalum



Wanafunzi wa shule ya msingi uhuru mchanganyiko wakiimba wimbo maalum

Na Lilian Lundo

Serikali imenunua vifaa vya kufundishia na visaidizi kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu wa kusikia, kuona na wenye ulemavu wa akili huku ikiendelea kuboresha mfumo wa elimu nchini.

Hayo yamebainishwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa katika hotuba yake ya kuahirisha mkutano wa Sita wa Bunge la Kumi na Moja mapema mwezi huu, Mjini Dodoma.

“Serikali imenunua vifaa vya kufundishia na visaidizi kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu wa kusikia, kuona na wenye ulemavu wa akili, vifaa hivyo vinajumuisha mashine 932 za maandishi ya nukta nundu, rimu za karatasi za breli zipatazo 2,548 na shime sikio (hearing aids) 1,150,”

alifafanua Mh.Kassim Majaliwa.

Aliendelea kusema kuwa, katika kutekeleza dhana ya elimu jumuishi pia Serikali imenunua vifaa kwa ajili ya upimaji ili kubaini mahitaji mbalimbali ya kujifunzia kabla na baada ya usajili wa watoto katika shule za msingi.

Mh. Majaliwa amesema kuwa vifaa vya watoto wenye mahitaji maalum ambavyo vimegharimu kiasi cha shilingi bilioni 3.6 vimekwishapokelewa na vitasambazwa katika shule zenye wanafunzi wenye mahitaji maalum kuanzia Machi 1, 2017.

Aidha amesema kuwa kutokuwepo kwa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu imekuwa ni changamoto kwao katika

kujifunza kwa ufanisi.

Waziri Mkuu pia aliwataka wazazi wenye watoto wenye mahitaji maalum kuwapeleka shule badala ya kuwaficha majumbani. Wakati huohuo Mh. Majaliwa alisema Serikali inaendelea na jitihada za kuhakikisha upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia na hadi sasa Serikali imefanikiwa kusambaza nakala 6,862,800 za vitabu vya kiada kwa Darasa la kwanza vya Mtaala uliobereshwa wa shule zote za msingi Tanzania Bara.

Vile vile uchapaji wa vitabu vya Darasa la pili nakala 6,862,800 unaendelea na uchapishaji wa nakala 6,818,181 za Darasa tatu umekamilika ambapo nakala hizo za Darasa la Tatu zitasambazwa sanjari na vifaa vya Darasa la Pili.

Kwa upande wa shule za Sekondari nakala 2,109, 683 zimechapishwa na usambazaji umeanza Februari 7, 2017.

Pia Serikali imeagiza vifaa vya maabara kwa ajili ya shule 1,625 za Sekondari nchini ambapo hadi sasa asilimia 70 ya vifaa hivyo imekwishawasili nchini na usambazaji wake umeanza hivi karibuni katika kanda ya Dar es Salaam.

Waziri Mkuu amesema kuwa vifaa hivyo viwe chachu ya wanafunzi kuchangamkia masomo ya sayansi na hivyo kulifanya Taifa kutengeneza wanasayansi wengi zaidi .

Kanuni za Sheria ya Huduma za Habari Zanza Kutumika Rasmi



Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Nape Moses Nnauye akioongea na Waandishi wa Habari kuhusu kutumika kwa Sheria ya Huduma za Habari ya Mwaka 2016 pamoja na Kanuni zake za 2017 katika Ukumbi wa Idara ya Habari Bungeni Mjini Dodoma 05/02/2017. Kushoto ni Mkurugenzi wa Idara ya Habari (MAELEZO) Dkt. Hassan Abbasi.

Na Jovina Bujulu

Kanuni za Sheria ya Huduma za Habari 2016 zimeanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la serikali.

Kanuni hizi zitasaidia kutambuliwa na kuheshimika kwa sekta ya habari kama taaluma rasmi inayofuata weledi kama zilivyo taaluma nyingine.

Akizungumza kuhusu kanuni za sheria hiyo Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo ambaye pia ni msemaji Mkuu wa serikali kwa mujibu wa sheria na kanuni hizo, Dkt Hassan Abbasi alisema kwamba ni kanuni ambazo zimekuja wakati Muafaka kwani zitasaidia sana katika utekelezaji wa sheria hiyo.

“Kanuni hizo ndio moyo wa mafanikio ya sheria hiyo na zitasaidia kufikia azma ya serikali ya kuwa na taaluma ya habari

inayoheshimika na kukubalika kama zilivyo tasnia nyingine hapa nchini” Alisema Dkt. Abbasi.

Kanuni za Sheria ya huduma za habari ya mwaka 2016 zimeanza kutumika rasmi tarehe 3 Februari, 2017 baada ya kusainiwa na Waziri mwenye dhamana pamoja na kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Kwa mujibu wa kanuni hizo vitambulisho kwa wanahabari (Press Card) vitaendelea kutolewa kwa utaratibu uliokuwa ukutumika awali hadi hapo bodi ya ithibati itakapoundwa.

Naye Kaimu Msajili wa Magazeti Patrick Kipangula alisema kanuni hizo zinaweka kiwango cha elimu kwa waandishi wa habari ambapo kwa sasa itakuwa ni kuanzia ngazi Stashahada.

Pia alisema kwa mujibu wa utaratibu wa kanuni za Sheria ya hudumazahabariyamwaka2016

vitambulisho vya wanahabari (press card) vitatolewa kila baada ya miaka miwili badala ya mwaka mmoja kama ilivyokuwa katika utaratibu wa awali.

Katika Sheria hiyo ili mwana habari atambulike na kupatiwa kitambulisho cha kuwa mwana habari “press card” ni lazima awe ana elimu ya kuanzia Stashahada, lakini kwakuwa sheria hiyo imeanza kutumika wakati wanahabari wengi wakiwa hawana sifa za kutosha, Sheria inatoa muda wa kujiandaa wa miaka mitano tangu kuanza kutumika kwa sheria hiyo ili kila mmoja anayetaka kuendelea kufanya kazi ya uandishi wa habari akasome kwa ajili ya kufikia kiwango hicho kinachotambuliwa.

Aidha alisema kanuni hizo zinaweka mfumo mzuri na rafiki kwa umiliki wa vyombo vya habari ambapo Watanzania wamepewa haki

ya kumiliki vyombo vya habari kwa asilimia 100 na wageni wamepewa asilimia isiyozidi 49.

Kanuni zitasaidia waandishi wa habari kuwa na weledi wa msingi ya maadili ya taaluma ya habari na Jamii hivyo wataepuka kufanya makosa ambayo ni

kinyume cha taaluma ya habari. Kuanza kutumika kwa sheria ya huduma za habari kumefuta sheria ya Magazeti ya mwaka 1976 ambayo imekuwa ikilalamikiwa na wadau mbalimbali wa habari na imekuwepo kuwa zaidi ya miaka 40. Kwa upande wake waziri

mwenye dhamana ya Habari Mh.Nape Nnauye alitoa wito kwa wanahabari kuisoma sheria na kanuni zake kwa kina ili kama watabaini kuwa kuna dosari za msingi ambazo zinahitaji marekebisho wasisite kuwasiliana na wizara ili kuona utaratibu wa kufanya marekebisho.

Mazoezi ni Tiba kwa Magonjwa Yasiyoambukiza –Makamu wa Rais



Makamu wa Rais Mh.Samia Suluhu Hassan akishiriki mazoezi mapema mjini Dodoma ikiwa ni sehemu ya kumuunga mkono Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa katika Uzinduzi wa Kitaifa wa Mazoezi ya Viungo kwa wananchi wote ya kupambana na magonjwa yasiyoambukiza,

Na Georgina Misama

Hivi karibuni viongozi mbalimbali wa Kitaifa wameshiriki mazoezi mbalimbali na kuwahamasisha wananchi kufanya mazoezi kwa ajili kupunguza uwezekano wa kupata

magonjwa yasiyoambukiza.

Hatua hiyo ililenga kuwajengea watazania kuwa na utamaduni wa kufanya mazoezi ikiwa ni njia ya kuimarisha afya na kupunguza magonjwa yasiyoambukizwa kama vile

kisukari, shinikizo la damu, kansa na magonjwa ya njia ya hewa. Jitihada hizo za viongozi waandamizi waliopo madarakani na wastaafu zinaunga mkono kampeni iliyozinduliwa katikati ya Disemba mwaka jana na Wizara ya Afya Maendeleo



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa (aliyevaa traksuti nyeupe) akiwa ameongozana na Viongozi mbalimbali kwenye Mazoezi ya Viungo kwa Wananchi wote yaliyofanyika Uwanja wa Jamhuri mjini Dodoma

ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ya kupambana na magonjwa yasioambukiza kwa kufanya mazoezi.

Kampeni hizo zilizinduliwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan na Waziri wa Afya, Ummu Mwalimu kwa kuongoza mazoezi ya kutembea yaliyoanzia viwanja vya Chuo cha Muhimbili na kumalizia Viwanja vya Leaders Club

Mbali na matembezi yalioongozwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia, naye Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akishiriki matembezi ya mazoezi ya viungo kwa Mawaziri Wabunge pamoja na wananchi yaliyofanyika katika Uwanja wa Jamhuri Dodoma yakiwa na lengo la kupambana na maradhi yasiyo ambukizika Mazoezi hayo yamefanyika kitaifa Mkoani Dodoma.

Akizungumza katika mazoezi

haya Waziri Mkuu aliziagiza Halmashauri, Manispaa na Majiji yote nchini kutenga maeneo kwa ajili ya watu kufanya mazoezi na kupumzika.

“Ni muhimu kufanya mazoezi kila siku, mazoezi yanasaidia kuchangamsha mwili, kufahamiana, kujenga urafiki pamoja na kuwa na afya bora,” alifafanua Kassim Majaliwa.

Aidha, Kassim Majaliwa alisema kwamba mwikio wa ufanyaji mazoezi ya viungo ni mkubwa, watu wengi wamejiunga na vikundi mbalimbali vya kufanya mazoezi ya viungo na kuzitaka Halmashauri, Manispaa na Majiji yote nchini kutenga maeneo kwa ajili ya watu kufanya mazoezi na kumpizika.

Katika kuonyesha kuwa wananchi wako tayari kuna vikundi mbalimbali vya mazoezi vinavyosimamiwa na Maafisa Utamaduni na Maafisa Michezo kutoka Manispaa ya Ilala, Kinondoni

na Temeke kwa Jiji la Dar es Salaam ambavyo vimeundwa ili kuhamasisha wakazi wa maeneo husika kufanya mazoezi katika kuimarisha afya zao. Sanjari hiyo, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ili kuunga mkono jitihada za viongozi mbalimbali za Serikali iliratibu bonanza lililoandaliwa na Chama Cha Maafisa Mawasiliano Serikalini, Wahariri wa Vyombo vya Habari nchini pamoja na Chama Cha Waandishi wa Habari Dar es Salaam.

Lengo la Bonanza lile ilikuwa kuhamasisha wadau wa habari kuchangia damu, kupima afya pamoja na kufanya mazoezi ya viungo katika kuimarisha afya zao, ambapo wakazi wote wa Jiji la Dar es Salaam walialikwa kushiriki bonanza hilo.

Mwitikio kutoka kwa wadau wa habari waliopo Jijini Dar es Salaam haukuwa mzuri, na sio kwa wadau wa habari tu, bali hata kwa wananchi kwa ujumla.

Ni kutokana na hali niliyoiona nimeshawishika kuchukua kalamu na kuwasih watazania wenzangu, tujenge utamaduni wa kutumia vyema fursa kama hizo za kufanya mazoezi na kupima afya bila malipo kila zinapotokea.

Najiuliza Watanzania tunahitaji msada gani juu ya swala la kuimarisha afya zetu kwa kupima na kufanya mazoezi, ni watanzania wangapi wamekuwa wakilalamikia gharama kubwa za vipimo na matibabu katika hospitali zetu, na kwa nini tusubiri kuumwa ikiwa tunaweza kujizuia bila gharama.



Welcome to Generation T.Solved



LIMEANDALIWA NA

Idara ya Habari-MAELEZO

S.L.P 8031

Dar es Salaam-Tanzania

Simu : (+255) 22 -2122771

Barua pepe: maelezo@habari.go.tz

Tovuti: www.tanzania.go.tz



@TZ_MsemajiMkuu



Msemaji Mkuu wa Serikali



Habari Maelezo